# HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

*(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

Mkoa wa Arusha,
Telegram: Arusha,
Simu: 073 6500476,
Faksi: 250 3701,
Email:ded@arushadc.go.tz

Ukumbi wa Halmashauri,
S.L.P.2330,
**ARUSHA**

Kumb. Na. MM/AR/S20/12/145

21.03.2018

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya Arusha anapenda kuwatangazia Watanzania wenye sifa na uwezo kuomba nafasi za kazi **25** za **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III (VILLAGE EXECUTIVE III)**

## 1.1 Kazi/majukumu ya kufanya

(i) Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji
(ii) Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji
(iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
(iv) Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
(v) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
(vi) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
(vii) Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji
(viii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji
(ix) Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika kijiji
(x) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
(xi) Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji
(xii) Atawajibika kwa mtendaji wa kata

## 1.2 Sifa za kuajiriwa

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyemaliza mafunzo ya Astashahada katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

Scanned by CamScanner

**1.3 Mshahara**

Ngazi ya mshahara wa serikali TGS B.

**2.0 Masharti ya ujumla**

(i) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45

(ii) Waombaji waambatanishe barua ya maombi iliyoandikwa kwa mkono, nakala za vyeti vya elimu na taaluma, cheti cha kuzaliwa, wasifu (CV) na pasiporti ya hivi karibuni.

(iii) Maombi yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza

(iv) Waombaji watakao wasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria

(v) Hati za matokeo hazitakubalika

(vi) Waombaji waliofukuzwa kazi na wenye kesi za jinai wasiombe nafasi hizi

**(vii) Mwisho wa kutuma maombi ni siku 14 tangu kutoka kwa tangazo hili gazetini**

**(viii) Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA**

***(ix)*** Maombi yote yatumwe kwa:

***MKURUGENZI MTENDAJI,***
***HALMASHAURI YA WILAYA ARUSHA,***
***S.L.P. 2330***
***ARUSHA***

***(x)*** Tangazo hili linapatikana pia kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha www.arushadc.go.tz na kwenye mbao za matangazo za Halmashauri ya wilaya ya Arusha

Paulus B. Kessy
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA

Scanned by CamScanner